

## Maswali

1. Mbona watu wa ukoma walilazimika kuishi mbali na watu wengine?
2. Watu wa ukoma walibeba nini?
3. Yesu alikutana na watu wa ukoma wangapi?
4. Watu wa ukoma walipiga kelele eti nini?
5. Mtu wa ukoma akiwa sawa alikuwa afanye nini?
6. Yesu alifanya nini?
7. Yesu aliambia watu wa ukoma wafanye nini?
8. Nini ilifanyika wakati watu wa ukoma walienda kujionyesha kwa kuhani?
9. Watu wa ukoma walienda wangapi kushukuru Yesu?
10. Yesu aliambia huyu mtu wa ukoma aliyerudi kwake eti nini?

## Majibu

1. Kwa sababu ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya na ungeambukisha.
2. Watu wa ukoma wangebeba kengele iliyohadharisha watu wasiwakaribie.
3. Yesu alikutana na watu 10 wa ukoma.
4. ‘Yesu, Bwana, uturehemu.’
5. Alienda kujionyesha kwa kuhani ili amuangalie kamaako vizuri tena.
6. Yesu alienda karibu na watu wa ukoma.
7. Yesu aliambia waende kujionyesha kwa kuhani.
8. Walipokuwa wakienda kwa kuhani, walipona.
9. Mtu wa ukoma mmoja tu ndiye alienda kumshukuru Yesu.
10. ‘Enenda zako. Imani yako imekuponya.’

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 39 Yesu anaponya watu 10 wa ukoma

## Marejeo

Luka 17: 11 – 19

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu ana uwezo wa kuponya magonjwa. Yesu anafurahia watu wakimshukuru Mungu na kumpa utukufu.

## Maneno maalum

- 39.1 Ukoma + vidonda mbaya vya ngozi + mbali na watu + kengele + najisi
- 39.2 Yesu + wa ukoma kumi + ‘Uturehemu’ + Yesu alienda karibu + kuhani + chunguza + Yesu + ‘Enda kwa kuhani.’
- 39.3 Wa ukoma kumi + amini + enda + kuhani + vizuri tena
- 39.4 Wa ukoma mmoja + rudi nyuma kwa yesu + ‘Asante’ + Yesu alifurahi + kuhani + vizuri + furahi sana

**39.1** Kwa nchi ya Israeli, kulikuwa na watu waliokuwa na ugonjwa mbaya wa ngozi uitwao ukoma. Watu wa huu ugonjwa waliitwa watu wa ukoma. Ulikuwa ugonjwa mbaya sana. Madaktari hawakuweza kuuponya. Kama wangeguza mtu, huyo naye angeshikwa na huo ugonjwa. Watu wa ukoma waliishi mbali na watu wengine. Hawakukubaliwa kwenda karibu na watu wazima. Watu wa ukoma walitembea na kengele ikipiga ili watu wawahebe.

**39.2** Siku moja Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wanaenda Yerusalem, waliona kijiji kimoja kwa umbali. Karibu na kijiji, Yesu aliona watu kumi. Walikuwa wakipiga kengele na kelele ili watu wasikuje karibu nao kwa sababu walikuwa na ukoma. Watu waliwapelekea chakula kule kwa kijiji lakini walijihadhari wasiende karibu nao ili wasishikwe na ukoma. Walikuwa wakiwawekea chakula chini. Baada ya wao kuenda, watu wa ukoma wangekuja na wachukue hicho chakula.

Watu wa ukoma walipoona Yesu na wanafunzi wake, waliita kwa sauti, "Yesu, Bwana mkubwa, uturehemu." Walikuwa wamemuona Yesu hapo awali, na walisikia kwamba anaponya watu. Watu wengi walitoroka watu wa ukoma lakini Yesu hakuwaogopa.



Yesu alienda karibu na wale watu kumi wa ukoma. Aliuja kwamba wale watu wa ukoma wakiwa wazima, lazima kuhani wa hekalu awaangalie kama wako vizuri kabisa. Halafu wataenda nyumbani kuwa na watu wengine. Kwa hivyo Yesu aliwambia, "Enda mijionyeshe kwa kuhani."

**39.3** Wale watu wa ukoma waliamini Yesu kwa hivyo walifanya vile aliwambia. Walianza kwenda kumtafuta kuhani. Walipokuwa wakienda kwa kijiji, walijiangalia na wakaona wako vizuri tena. Ngozi yao ilikuwa mzuri tena, nyororo kama zamani. Waliangalia na kujisikia sana. Walikuwa waende kwa familia zao na marafiki wao baada ya kumuona kuhani. Tisa wao walienda haraka kumuona kuhani na kujionyesha kuwa wako vizuri.

**39.4** Mmoja wa hao wa kumi, alijuwa anatakiwa aende kwa kuhani lakini alifikiria juu ya Yesu vile alikuja kwenye walikuwa na akamponya. Kwa hivyo huyu wa kumi alikimbia akarudi kwa Yesu. Njiani alimsifu Mungu kwa kuwa mzima tena.

Huyo wa kumi wa ukoma aliporudi kwa Yesu, alianguka chini mbele ya Yesu na kumshukuru. Yesu alishangaa mbona wale wengine tisa hawajarudi kumshukuru, lakini alifurahia yule mmoja aliyekumbuka kuja kumshukuru. Yesu kwa upole aliambia yule mtu, "Simama na uende kwa sababu imani yako imekuponya."



Halafu huyo mtu alienda kwa kuhani k u m w o n y e s h a kwamba amepona. Baadaye akaenda nyumbani kama amefurahi sana.